## NUKUU WIKI HIKI

**WAZIRI MKUU MIZENGO PINDA**
"Tuwaunge mkono wagombea wanaokubalika na wenye sifa ya kutuletea maendeleo tofauti na hivyo, tukifanya makosa tutaanguka asubuhi tena anguko la mwereka." Kauli hiyo aliitoa Februari 19 mwaka huu.



**DK. FENELLA MKANGARA**
"Viongozi wanaosimama na kusema kwamba vijana ni bomu linalosubiri kulipuka, ni watu wa ovyo ovyo na wananikera." Kauli hii aliitoa Februari 20 mwaka huu.



**JAJI DAMIAN RUBUVA**
"Viongozi wa siasa wasitumie mwanvuli wa BVR kutaka kufanya fujo, bali watumie nafasi hii kuwahamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha."Kauli hii aliitoa Februari 20 mwaka huu.

# Serikali yashutumiwa kwa ukatili

NA ELIAS MSUYA, DAR ES SALAAM

CHAMA cha kimataifa cha kutetea jamii za watu wanaoishi karibu na hifadhi za taifa (Indigenous peoples' and community conserved territories and areas - ICCAs) kimeishutumu Serikali ya Tanzania kwa kuwafukuza kutoka kwenye makazi yao wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya hifadhi.

ICCA imeiandikia Serikali barua iliyojaa shutuma ikieleza kuwa kilichofanyika ni kitendo ambacho ni kinyume na haki za binadamu.

Katika taarifa yake ya Februari 17 iliyotoka siku chache baada tukio hilo, ICCA yenye makao yake makuu Geneva, Uswisi, imeitaja operesheni iliyofanywa na Serikali katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ya kuviondoa vijiji vya Ololosokwan na Arash, vilivyopo Loliondo wilayani Ngorongoro, Mkoa wa Arusha kwa kuchoma moto makazi ya wananchi kwa madai ya kuvamia eneo la hifadhi kuwa haikuwa ya utu.

Sehemu ya taarifa hiyo ilieleza: "Ieleweke kwamba uharibifu huu wa mali umeripotiwa kufanyika nje ya mipaka ya hifadhi kwenye ardhi za vijiji. Ndicho kilichotokea Loliondo na imekuwa chanzo cha migogoro baina ya mamlaka za Serikali na wanavijiji ukiwamo mgogoro wa mwaka 2009.

"Mgogoro ulioripotiwa Loliondo ni ukatili ulioshtua katika sera za Serikali za hifadhi na vyombo vya sheria na wanajamii. Maeneo mengine ambayo yamekuwa katika mizozo kama hiyo ni pamoja na Kijiji cha Kimotorok karibu na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, bonde la Mto Kilombero na Bonde la Usangu lililo karibu na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha."

Rekodi zilizopo zinaonyesha kuwa mwaka 2013 eneo hilo hilo lilihusishwa katika mgogoro wa kitaifa na kimataifa baada ya Serikali ya Tanzania kudaiwa kutaka kuligeuza kuwa pori la akiba na kuwaondoa wananchi wapatao 25,000. Hata hivyo, Waziri Lazaro Nyalandu alikanusha taarifa hizo kwa kile alichoeleza kuwa ni uzushi.

Kwa mujibu wa ICCA, eneo la Ngorongoro lenye zaidi ya watu 60,000 lina uhaba wa chakula kutokana na vikwazo vya kufanya shughuli za kibinadamu vilivyowekwa na Serikali kwa wenyeji wa eneo hilo kwa sababu ni la urithi wa dunia.

### Kauli ya Serikali

Akizungumzia operesheni iliyofanyika Loliondo hivi karibuni, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Adelhelm Meru, alisema Serikali haikuchoma nyumba za wananchi bali ilichokichoma ni mabanda ya wafugaji.

"Hakuna nyumba iliyochomwa pale wala hakuna mtu aliyevunjiwa nyumba. Yale ni mabanda tu, si unajua tena wafugaji wana tabia ya kujenga mabanda na kuhamishia mifugo yao kwenye hifadhi? Halafu wakiachwa wanahamia hapo.

"Tulichofanya ni kuwafukuza na kuyavunja mabanda kwa kutumia kikosi cha Tanapa. Hakuna aliyeumia wala hakuna aliyekufa, ni amani tu," alisema Dk. Meru.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Liberatus Sabas, alipoulizwa kuhusu hilo, alisema hana taarifa ya kuwapo kwa operesheni hiyo.

### Vitongoji vya hifadhi ya Saadani

Hivi karibuni, chama hicho kiliiandikia barua mbili Serikali ya Tanzania ikiilaumu kwa kutaka kukihamisha Kitongoji cha Uvinje kilichopo katika Hifadhi ya Saadani, Wilaya ya Bagamoyo.

Katika barua hizo mbili, ya Agosti 14, 2014 na ya Februari 5, 2015, chama hicho kimepinga hatua ya Serikali kuwahamisha wananchi kwenye kitongoji hicho kwa kuwa ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

Barua hizo zimetumwa kwa Rais Jakaya Kikwete, Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Waziri wa Maliasili na Utalii, Lazaro Nyalandu, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maliasili, Mazingira na Utalii, James Lembeli, aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Profesa Anna Tibaijuka na Mkurugenzi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Allan Kijazi.

Uvinje ni miongoni mwa vitongoji vinane vya Kijiji cha Saadani na Serikali ilitaka kukiondoa tangu mwaka 2005 baada ya kuipandisha daraja Hifadhi ya Saadani kutoka pori la akiba na kuwa hifadhi kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 281 la Septemba 16, 2005.

Hata hivyo, wananchi wa kitongoji hicho wanadai Rais Kikwete alifika kijijini hapo kabla ya kugombea urais mwaka 2005 na kuwahakikishia kuwa hawataondolewa.

Akizungumzia suala hilo mwishoni mwa mwaka jana, Mhifadhi Mkuu wa Saadani, Hassan Malungu, alisisitiza kitongoji hicho kimo ndani ya hifadhi kinyume cha sheria na kwamba mambo ya siasa ndiyo yamechelewesha kukiondoa.

Alisisitiza kuwa sheria za hifadhi za taifa haziruhusu kuwa na makazi ya watu ndani yake.

"Kwa ufupi tu ukiangalia GN (Tangazo la Serikali) linaonyesha kuwa eneo lote la Kitongoji cha Uvinje liko ndani ya hifadhi. Ni kweli lilikuwa eneo la watu ambao walikuwa watumishi wa pori la akiba tangu lilipoanzishwa mwaka 1968. Waliombwa kuondoka, lakini waliendelea kuongezeka," alisema Malungu.

Moja ya barua hizo za ICCA, inasomeka: "Tanzania inayoongoza duniani katika uhifadhi ambapo robo ya eneo lake lote ni hifadhi za taifa na maeneo tengefu, lakini sasa imegeuka kuwa eneo la migogoro, kati ya Serikali, sekta binafsi na wanajamii wanaozunguka maeneo hayo. Ni wazi kwamba matukio haya yanachafua sifa hiyo.

"Migogoro hii ina matokeo mabaya kwa uhifadhi wa taifa na mapato ya nchi, hasa kwa kuwa utalii unaiingizia Tanzania jumla ya dola za Marekani bilioni mbili kwa mwaka."

Sehemu nyingine ya moja ya barua hizo za ICCA imekumbushia pia mkutano wa Novemba, 2014 uliofanyika Sydney nchini Australia ambao zaidi ya watu 6,000 kutoka duniani wakiwamo wawakilishi wa Tanzania walihudhuria kwa ajili ya kuweka mikakati na hatua za uhifadhi kwa muongo unaokuja.

Inasomeka: "Tanzania ni mfano hai katika hili. Si chini ya vijiji 1,233 vimekuza hekta 2.366 milioni za miti na misitu na uoto wa asili kama maeneo yanayotunzwa na vijiji. Isitoshe, hekta 5.392 milioni za taifa na maeneo ya vijiji yamekuwa yakitunzwa na wanavijiji.

"Asilimia tatu ya nchi yote iko chini ya jumuiya za hifadhi za wanyamapori (WMA) 38, ziliyotengwa na vijiji 148 kwa ajili ya hifadhi za wanyamapori yakiwa yanatunzwa na watu wapatao 440,000."

Hata hivyo, Katibu Mkuu, Dk. Meru aliyeingia wizarani hapo mwishoni mwa mwaka jana, alisema bado hajaziona barua hizo.

"Siwezi kuwa na jibu zuri kwa kuwa sijaziona barua zenyewe. Ila niseme tu kwamba watu wamekuwa na tabia ya kuvamia maeneo ya Serikali. Ardhi inauzwa bei ghali, hivyo mtu anaona njia rahisi ni kuvamia maeneo ya Serikali yawe ya misitu au hifadhi," alisema Dk. Meru.

### Ujangili wa meno ya tembo

ICCA haikuacha kuinyooshea kidole Tanzania kwa tatizo la ujangili wa meno ya tembo, ikisema zaidi ya asilimia 50 ya tembo wameuawa kwa ujangili.

"Kama hiyo haitoshi, Tanzania imekuwa maarufu kwenye vyombo vya habari vya kimataifa kwa tatizo la ujangili. Karibu asilimia 50 ya tembo wake wamepotelea kwenye janga hilo huku Serikali na sekta binafsi vikihusishwa na mauaji ya wanyama kutokana na athari yake katika utalii.

"Kuwaondoa watu wanaomiliki kihalali maeneo yaliyo karibu na hifadhi zilizo maarufu kimataifa na kuchoma nyumba zao ni kitendo cha aibu," ilisema ICCA.



Wakazi wa Ololosokwan wakiangalia mabaki ya boma lililochomwa.